**TAARIFA YA UTENDAJI WA VIWANDA VYA KUSINDIKA MKONGE KWA KIPINDI CHA MWEZI MACHI HADI DISEMBA 2021**

## 1.0 UTANGULIZI

Kampuni ya Sisalana ni moja ya kampuni za kitanzania ambayo inamilikiwa na mfuko wa hifadhi ya jamii (yaani NSSF) kwa asilimia 100%. Kampuni ya Sisalana ilianza shughuli zake ya utendaji tarehe 12. 03. 2021, Kampuni ya Sisalana inamiliki viwanda saba vya kuchakata Majani ya Mkonge (yaani kiwanda cha Magunga, Mwelya, Usambara, Hale, Ngombezi, Magoma Songea na Magoma Kulasi) ambapo majani hayo hutoka kwa wakulima kupitia usimamizi wa AMCOS tano (Magoma AMCOS, Magunga AMCOS, Hale AMCOS, Mwelya AMCOS, na Ngombezi AMCOS).

Ikumbukwe kwamba, Kampuni ya Sisalana ilianzishwa kwa lengo la kusimamia mali zote zilizochukuliwa na NSSF kutoka kwa Kampuni ya Katani baada ya kampuni tajwa kushindwa kulipa madeni yake kwa NSSF. Hivyo mali zote zilizokuwa dhamana ya mikopo iliyotolewa na NSSF kwa Kampuni ya Katani ikihusisha viwanda hivyo saba vya usindikaji vilichukuliwa na sasa vinasimamiwa na NSSF kupitia kampuni yake ya Sisalana.

Mara baada ya kuchukua mali hizo, kwa maelekezo ya Serikali NSSF haikupaswa kusimamisha shughuli za uzalishaji hivyo hatua za haraka zilichukuliwa ikiwemo kutengeneza mpango kazi wa muda mfupi kuendeleza uzalishaji katika kipindi cha mpito. NSSF ililazimika kuchukua hatua hii kwa sababu yenyewe katika uwekezaji hua kuna miongozo ya kuifuata inayotolewa na benki Kuu ya Tanzania na moja wapo ni kwamba lazima upembuzi yakinifu ufanyike kuangalia tija ya uwekezaji kabla ya kuweka. Hivyo mchakato wa kuanza kwa upembuzi yakinifu ulishafanyika na sasa upembuzi unaendelea na uanatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Machi 2022.

Aidha, NSSF ilichukua hatua za haraka za kunusuru kazi ziendelee kwa kipindi cha mpito cha kusubiria upembuzi yakinifu ukamilike, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kutoa mtaji kiasi kwaajili ya uboreshaji wa miundombinu ya uzalishaji ikiwemo ukarabati mkubwa wa Makorona ambao ulikua haujafanyika kwa zaidi ya miaka saba iliyopita; ujenzi wa vichanja vipya vya chuma ili kukidhi mahitaji halisi ya kila kiwanda na ukarabati wa vichanja vilivyokuwa vimeharibika; na kuboresha hali ya maslahi ya wafanyakazi ili kuwapa ari ya kufanya kazi kwa ufanisi ikiwemo kulipa stahiki zao kwa wakati, kulipa michango yao ya NSSF, kupata bima ya matibabu, kulipia kodi ya mapato, kuchangia Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), kwa Chama cha Wafanyakazi (TPAWU) na kuwapatia vifaa vya kazi. Hadi taarifa hii inaandikwa ukarabati wa makorona ulishafanyika kwa viwanda vyote isipokuwa Hale ambao AMCOS yao ilishauri tusubiri kidogo wafidie uzalishaji uliokuwa umepotea walipokuwa wamepata changamoto ya Korona kwa vipindi viwili tofauti. Taarifa kamili ya ukarabati wa Makorona nayo imeambatishwa kwaajili ya urahisi wa kurejea.

Taarifa hii imebeba utendaji wa viwanda saba vya kusindika mkonge vinavyomilikiwa na kampuni ya Sisalana katika kipindi cha mwezi machi hadi mwezi Disemba 2021. Aidha taarifa hii itaonyesha pia ulinganisho wa uzalishaji ulio fanyika katika kipindi cha kipindi kama hicho kwa mwaka 2020 kabla ya kuanzishwa kwa Sisalana kwaajili ya kupima maendeleo ya usindikaji mkonge katika viwanda hivyo.

## 2.0 USINDIKAJI WA MAJANI YA MKONGE

### 2.1 LENGO LA USINDIKAJI NA MAFANIKIO

Katika kipindi cha mwezi Machi hadi mwezi Disemba 2021 kampuni ilikuwa na lengo la kusindika jumla **meta 188,444.33**, kulainisha na kufunga **tani 6,275.86**. Uhalisia wa uzalishaji ni **meta 140,286.78** kati ya meta 140,444.69 zilizoletwa viwandani ambapo ni sawa na **asilimia 74** ya lengo. Kwa upande wa ulainishaji na ufungaji uhalisia ni **tani 4,623.28** sawa na **asilimia 73** ya lengo kwa kipindi cha mwezi Machi hadi Disemba 2021.

Taarifa imeambatanishwa kama ifuatavyo: -


(a) Uzalishaji -katika kipindi cha mwezi Machi hadi Disemba 2021 kiwanda cha Hale kimeongoza katika uzalishaji kikifuatiwa na kiwanda cha Magunga kwa kupata jumla ya asilimia 99% na 87% ya lengo la uzalishaji lilowekwa na Kampuni. Sambamba na hivyo pia uzalishaji umeongeka kutoka asilimia 71% kwa mwaka 2020 hadi asilimia 74% kwa mwaka 2021 kwa upande wa usindikaji lakini pia kwa upande wa uzalishaji watani umeongezeka kutoka asilimia 71% kwa mwaka 2020 hadi asilimia 73% kwa mwaka 2021. Hivyo ongezeko ni 3% kwa 2% kwa mfuatano. Takwimu zimeonyeshwa hapo chini katika jedwali namba 1.

**Jedwali namba 1: Takwimu za Usindikaji, Ulainishaji na Ufungaji**


| UTENDAJI WA USINDIKAJI WA VIWANDA KWA KIPINDI CHA MACHI HADI DISEMBA 2021 | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KIWANDA | 2020 | | | | 2021 | | | |
| | LENGO | HALISI | | | LENGO | HALISI | | |
| | | MTS REC | MTS DEC | (%) | | MTS REC | MTS DEC | (%) |
| HALE | 24,781.00 | 23,811.00 | 23,757.50 | 96% | 27,381.00 | 27,493.00 | 27,224.00 | 99% |
| NGOMBEZI | 25,100.00 | 19,082.00 | 20,157.50 | 80% | 26,599.00 | 21,604.00 | 21,499.50 | 81% |
| MAGUNGA | 25,100.00 | 21,016.50 | 21,020.00 | 84% | 24,932.33 | 21,708.50 | 21,649.50 | 87% |
| MAGOMA (KULASI & SONGEA) | 50,200.00 | 30,200.00 | 30,206.00 | 60% | 54,766.00 | 40,461.00 | 40,459.00 | 74% |
| MWELYA & USAMBARA | 50,200.00 | 29,749.59 | 29,821.51 | 59% | 54,766.00 | 29,178.19 | 29,454.78 | 54% |
| JUMLA | 175,381.00 | 123,859.09 | 124,962.51 | 71% | 188,444.33 | 140,444.69 | 140,286.78 | 74% |

| UTENDAJI WA UPINGAJI NA UFUNGAJI WA SINGA VIWANDA KWA KIPINDI CHA MACHI HADI DISEMBA 2021 | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KIWANDA | 2020 | | | | 2021 | | | |
| | LENGO | HALISI | | | LENGO | HALISI | | |
| | | ULAINISHAJI | UFUNGAJI | (%) | | ULAINISHAJI | UFUNGAJI | (%) |
| HALE | 854.52 | 854.75 | 848.50 | 99% | 912.70 | 874.15 | 858.50 | 94% |
| NGOMBEZI | 678.38 | 377.55 | 384.15 | 57% | 718.89 | 542.40 | 548.35 | 76% |
| MAGUNGA | 760.61 | 645.38 | 673.90 | 89% | 712.35 | 675.37 | 668.35 | 94% |
| MAGOMA (KULASI & SONGEA) | 1,930.77 | 1,209.00 | 1,302.00 | 67% | 2,106.38 | 1,616.75 | 1,617.25 | 77% |
| MWELYA & USAMBARA | 1,619.35 | 936.87 | 947.81 | 59% | 1,825.53 | 914.61 | 917.37 | 50% |
| JUMLA | 5,843.63 | 4,023.54 | 4,156.36 | 71% | 6,275.86 | 4,623.28 | 4,609.82 | 73% |

**Ufunguo:** MTS REC= Meta za majani ya Mkonge zilizofikishwa kiwandani; MTS DEC= Meta za majani ya Mkonge zilizosindikwa; Kipimo cha Ulainishaji na Ufungaji ni tani.




| | HALE | NGOMBEZI | MAGUNGA | MAGOMA (KULASI & SONGEA) | MWELYA & USAMBARA |
|---|---|---|---|---|---|
| 2,020 | 23,757.50 | 20,157.50 | 21,020.00 | 30,206.00 | 29,821.51 |
| 2,021 | 27,224.00 | 21,499.50 | 21,649.50 | 40,459.00 | 29,454.78 |




**(b). Uzalishaji wa madaraja ya singa**

Uzalishaji pia umezingatia madaraja ya singa yanayotokana na ubora wa majani yaliyosindikwa na umakini wa usimamizi wa wataalamu wa kiwanda Pamoja na wafanyakazi waliopo.

Ufanisi katika kuzalisha madaraja ya juu umeongezeka kwa kiasi kikubwa kwa mwaka 2021 ukilinganisha na madaraja ya Mkonge yaliyozalishwa mwaka 2020. Madaraja ya 3L, 3S haya hayakuzalishwa kabisa kwa mwaka 2020 kwa viwanda sita ila kwa mwaka 2021 yamezalishwa kwa viwanda vyote kwa asilimia 5 na 1 kutoka asilimia 0 kwa mwaka 2020. Vile vile uzalishaji wa daraja la UG uliweza kuongezeka kufikia asilimia 73 kutoka asilimia 53. Aidha uzalishaji wa madaraja ya mkonge ya chini yalipungua kwa kiasi kikubwa kwa kipindi cha mwaka 2021.

Takwimu kamili za uzalishaji wa madaraja mbali mbali ya Mkonge inaonekana katika majedwali mawili yanayofuta hapo chini (Jedwali namba mbili na namba tatu).

**Jedwali namba 2: Uzalishaji wa madaraja ya Mkonge; Brushing- Ulainishaji, Baling- Ufungaji**

| | PRODUCTION BY GRADES | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| BRUSHING 2020 | FACTORY | 3L | 3S | UG | SS UG | TOW I | TOWII | UF | TOTAL |
| | HALE | - | - | 383.65 | 405.55 | 22.50 | - | 43.05 | 854.75 |
| | NGOMBEZI | - | - | 240.55 | 110.50 | 9.40 | 2.60 | 14.50 | 377.55 |
| | MAGUNGA | 1.95 | - | 417.80 | 186.05 | 28.73 | 4.25 | 6.60 | 645.38 |
| | MAGOMA | - | - | 538.75 | 585.25 | 16.50 | 5.50 | 63.00 | 1,209.00 |
| | MWELYA & USAMBARA | - | - | 419.41 | 453.22 | 54.90 | 0.20 | 9.14 | 936.87 |
| | **TOTAL** | **1.95** | **-** | **2,000.16** | **1,740.57** | **132.02** | **12.55** | **136.29** | **4,023.54** |
| | | | | | | | | | |
| BRUSHING 2021 | FACTORY | 3L | 3S | UG | SS UG | TOW I | TOWII | UF | TOTAL |
| | HALE | 26.95 | 10.30 | 554.95 | 239.50 | 24.90 | - | 17.55 | 874.15 |
| | NGOMBEZI | 4.25 | 5.50 | 461.25 | 42.00 | 25.60 | 3.80 | - | 542.40 |
| | MAGUNGA | 150.70 | 24.60 | 409.30 | 58.18 | 29.39 | 0.90 | 2.30 | 675.37 |
| | MAGOMA | 2.25 | 0.50 | 1,315.75 | 236.75 | 32.00 | 1.00 | 28.50 | 1,616.75 |
| | MWELYA & USAMBARA | 35.95 | 25.05 | 604.50 | 217.74 | 28.49 | - | 2.88 | 914.61 |
| | **TOTAL** | **220.10** | **65.95** | **3,345.75** | **794.17** | **140.39** | **5.70** | **51.23** | **4,623.28** |
| | | | | | | | | | |
| BALING BY GRADES | | | | | | | | | |
| BALING 2020 | FACTORY | 3L | 3S | UG | SS UG | TOW I | TOWII | UF | TOTAL |
| | HALE | - | - | 384.50 | 399.75 | 22.50 | - | 41.75 | 848.50 |
| | NGOMBEZI | - | - | 249.70 | 101.75 | 15.60 | 3.60 | 13.50 | 384.15 |
| | MAGUNGA | 1.95 | - | 467.00 | 172.90 | 24.50 | 2.80 | 4.75 | 673.90 |
| | MAGOMA | - | - | 654.75 | 566.25 | 19.00 | 5.00 | 57.00 | 1,302.00 |
| | MWELYA & USAMBARA | - | - | 447.80 | 423.65 | 64.76 | 0.40 | 11.20 | 947.81 |
| | **TOTAL** | **1.95** | **-** | **2,203.75** | **1,664.30** | **146.36** | **11.80** | **128.20** | **4,156.36** |
| | | | | | | | | | |
| BALING 2021 | FACTORY | 3L | 3S | UG | SS UG | TOW I | TOWII | UF | TOTAL |
| | HALE | 25.75 | 10.00 | 554.25 | 226.75 | 24.50 | - | 17.25 | 858.50 |
| | NGOMBEZI | 4.25 | 5.25 | 459.85 | 44.85 | 29.40 | 3.50 | 1.25 | 548.35 |
| | MAGUNGA | 148.25 | 23.75 | 412.25 | 54.55 | 25.60 | 1.70 | 2.25 | 668.35 |
| | MAGOMA | 2.25 | 0.50 | 1,316.25 | 236.75 | 32.00 | 1.00 | 28.50 | 1,617.25 |
| | MWELYA & USAMBARA | 33.85 | 22.70 | 635.40 | 184.10 | 29.29 | 9.60 | 2.43 | 917.37 |
| | **TOTAL** | **214.35** | **62.20** | **3,378.00** | **747.00** | **140.79** | **15.80** | **51.68** | **4,609.82** |

**Jedwali namba 3: Ufupisho wa Madaraja ya mkonge yaliyozalishwa katika Ulainishaji na Ufungaji**

| MADARAJA YA SINGA | 2020 | | | | 2021 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ULAINISHAJI | UFUNGAJI | ULAINISHAJI (%) | UFUNGAJI (%) | ULAINISHAJI | UFUNGAJI | ULAINISHAJI (%) | UFUNGAJI (%) |
| 3L | 1.95 | 1.95 | 0.05% | 0.05% | 220.10 | 214.35 | 4.76% | 4.65% |
| 3S | - | - | 0.00% | 0.00% | 65.95 | 62.20 | 1.43% | 1.35% |
| UG | 2,000.16 | 2,203.75 | 49.71% | 53.02% | 3,345.75 | 3,378.00 | 72.37% | 73.28% |
| SS UG | 1,740.57 | 1,664.30 | 43.26% | 40.04% | 794.17 | 747.00 | 17.18% | 16.20% |
| TOW I | 132.02 | 146.36 | 3.28% | 3.52% | 140.39 | 140.79 | 3.04% | 3.05% |
| TOWII | 12.55 | 11.80 | 0.31% | 0.28% | 5.70 | 15.80 | 0.12% | 0.34% |
| UF | 136.29 | 128.20 | 3.39% | 3.08% | 51.23 | 51.68 | 1.11% | 1.12% |
| **JUMLA** | **4,023.54** | **4,156.36** | **100.00%** | **100.000%** | **4,623.28** | **4,609.82** | **100.0%** | **100.0%** |

## 3.0. CHANGAMOTO ZA UZALISHAJI

Katika kipindi cha mwezi Machi hadi mwezi Disemba, 2021, kumekuwa na changamoto na mbali mbali ambazo zimepelekea kutofika malengo ya uzalishaji kama ilivyokusidiwa katika malengo ya uzalishaji kwa Kampuni. Changamoto kubwa ambazo zilijitokea katika kipindi kilichotajwa ni kama ifuatavyo:

- Kukatika kwa umeme mara kwa mara au umeme mdogo kwa baadhi ya Viwanda;

- Miundombinu mibovu ya barabara na madaraja hasa msimu wa mvua unaopelekea kushindwa kuleta majani kiwandani au kutoa mzigo kiwandani;

- Matengenezo ya mitambo ya kusindikia majani ya mkonge, Ukarabati mkubwa wa mitambo ulipelekea kusimamisha uzalishaji kwa kipindi kisichopungua mwezi mmoja kwa kiwanda husika. Aidha, kutokana na mitambo yote kuwa ni kuu kuu kulikua na hali ya kuharibika kwa mitambo hiyo katika hali zisizotarajiwa kulingana na ratiba na mpango wa matengenezo.

- Mvua

- Wafanyakazi wa uzalishaji, kumekua na changamoto ya upatikanaji wa wafanyakazi hasa msimu wa kilimo ukifika au pale inapotokea uzalishaji umesimama kupisha matengenezo ya mitambo wafanyakazi wanapotea na inachukua muda na gharama kuwarejesha. Wafanyakazi wengine wamekuwa wakikimbia kazi wakilalamika kwamba kazi ya Mkonge ni ngumu hasa katika usindikaji.

- Kuchelewa kuletwa majani kiwandani. Hii inapelekea aidha kuchelewa kuanza kazi au kushindwa kufanya kazi kabisa katika siku husika.

Takwimu ya athari ya uzalishaji imeambatanishwa katika jedwali namba 4 lifuatalo hapo chini ambapo inaeleza changamoto tajwa hapo juu na namna zilizvyoathiri uzalishaji katika kipindi cha mwezi Machi hadi mwezi Disemba 2021.


**Jedwali namba 4: Changamoto za uzalishaji na athari zake katika uzalishaji.**

| CHALLENGES 2021 | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | KORONA BREAKDOWN (MASAA) | | | | MVUA | | UCHELEWAJI/KUT | REHABILIT | JUMLA YA |
| | | UMEME (MASAA | KAMBA | MKANDA | MOTA | MENGINEYO | (MM) | MASAA | OLETEWA MAJANI | ATION | MASAA |
| HALE | MASAA | 780.00 | 3.00 | - | 190.00 | 310.00 | 32.00 | 4.50 | - | - | 1,319.50 |
| | IDADI YA MTS | 9,750.00 | 37.50 | - | 2,375.00 | 3,875.00 | - | 56.25 | - | - | 16,093.75 |
| | MTS/TONS | 31.39 | | | 31.39 | 31.39 | | | | | 31.40 |
| | TONS | 310.58 | 1.17 | - | 75.66 | 123.44 | - | 1.76 | - | - | 512.61 |
| | | | KORONA BREAKDOWN (MASAA) | | | | MVUA | | UCHELEWAJI/KUT | REHABILIT | JUMLA YA |
| | | UMEME (MASAA | KAMBA | MKANDA | MOTA | MENGINEYO | (MM) | MASAA | OLETEWA MAJANI | ATION | MASAA |
| NGOMBEZI | MASAA | 111.00 | 1.50 | - | 53.00 | 138.00 | 45.12 | 159.24 | 27.00 | 458.00 | 992.86 |
| | IDADI YA MTS | 1,387.50 | 18.75 | - | 662.50 | 1,725.00 | - | 1,990.50 | 337.50 | 5,725.00 | 11,846.75 |
| | MTS/TONS | 37.00 | | | 37.00 | 37.00 | | 37.00 | 37.00 | 37.00 | 37.00 |
| | TONS | 37.50 | 0.51 | - | 17.91 | 46.62 | - | 53.80 | 9.12 | 154.73 | 320.18 |
| | | | KORONA BREAKDOWN (MASAA) | | | | MVUA | | UCHELEWAJI/KUT | REHABILIT | JUMLA YA |
| | | UMEME (MASAA | KAMBA | MKANDA | MOTA | MENGINEYO | (MM) | MASAA | OLETEWA MAJANI | ATION | MASAA |
| MAGUNGA | MASAA | 289.92 | 10.87 | 15.13 | 144.00 | 165.31 | 16.00 | 0.50 | 3.50 | 348.30 | 993.53 |
| | IDADI YA MTS | 3,624.00 | 135.88 | 189.13 | 1,800.00 | 2,066.38 | - | 6.25 | 43.75 | 4,353.75 | 12,219.13 |
| | MTS/TONS | 33.18 | 33.00 | 33.35 | 33.00 | 33.15 | | 33.00 | 33.00 | 33.00 | 33.08 |
| | TONS | 109.23 | 4.12 | 5.67 | 54.55 | 62.33 | - | 0.19 | 1.33 | 131.93 | 369.34 |
| | | | KORONA BREAKDOWN (MASAA) | | | | MVUA | | UCHELEWAJI/KUT | REHABILIT | JUMLA YA |
| | | UMEME (MASAA | KAMBA | MKANDA | MOTA | MENGINEYO | (MM) | MASAA | OLETEWA MAJANI | ATION | MASAA |
| MAGOMA | MASAA | 459.00 | 27.00 | 44.00 | 610.00 | 126.00 | 219.35 | 128.50 | 59.00 | 1,115.00 | 2,787.85 |
| | IDADI YA MTS | 5,737.50 | 337.50 | 550.00 | 7,625.00 | 1,575.00 | - | 1,606.25 | 737.50 | 13,937.50 | 32,106.25 |
| | MTS/TONS | 26.00 | 26.00 | 26.00 | 26.00 | 26.00 | | 26.00 | 26.00 | 26.00 | 26.00 |
| | TONS | 220.67 | 12.98 | 21.15 | 293.27 | 60.58 | - | 61.78 | 28.37 | 536.06 | 1,234.86 |
| | | | KORONA BREAKDOWN (MASAA) | | | | MVUA | | UCHELEWAJI/KUT | REHABILIT | JUMLA YA |
| | | UMEME (MASAA | KAMBA | MKANDA | MOTA | MENGINEYO | (MM) | MASAA | OLETEWA MAJANI | ATION | MASAA |
| MWELYA & USAMBARA | MASAA | 780.00 | - | - | 190.00 | 310.00 | 31.00 | 2.00 | 2.00 | - | 1,315.00 |
| | IDADI YA MTS | 9,750.00 | - | - | 2,375.00 | 3,875.00 | - | 25.00 | 25.00 | - | 16,050.00 |
| | MTS/TONS | 34.97 | | | 34.97 | 34.97 | | 36.00 | 36.00 | | 34.97 |
| | TONS | 278.84 | - | - | 67.92 | 110.82 | - | 0.69 | 0.69 | - | 458.97 |
| | | | KORONA BREAKDOWN (MASAA) | | | | MVUA | | UCHELEWAJI/KUT | REHABILIT | JUMLA YA |
| | | UMEME (MASAA | KAMBA | MKANDA | MOTA | MENGINEYO | (MM) | MASAA | OLETEWA MAJANI | ATION | MASAA |
| TOTAL | MASAA | 2,419.92 | 42.37 | 59.13 | 1,187.00 | 1,049.31 | 343.47 | 294.74 | 91.50 | 1,921.30 | 7,408.74 |
| | IDADI YA MTS | 30,249.00 | 529.63 | 739.13 | 14,837.50 | 13,116.38 | - | 3,684.25 | 1,143.75 | 24,016.25 | 88,315.88 |
| | MTS/TONS | 31.61 | 28.21 | 27.55 | 29.13 | 32.48 | | 31.16 | 28.95 | 29.19 | 30.50 |
| | TONS | 956.83 | 18.78 | 26.83 | 509.30 | 403.79 | - | 118.22 | 39.51 | 822.72 | 2,895.96 |

**Jedwali namba 4a: Ufupisho wa Changamoto na athari zake katika uzalishaji**

**MAJUMUISHO YA CHANGAMOTO ZA UZALISHAJI KWA UFUPI.**

| CHANGAMOTO | MASAA | MTS | TONS |
|---|---|---|---|
| UMEME | 2,419.92 | 30,249.00 | 956.83 |
| BREAKDOWN | 2,337.81 | 29,222.63 | 958.69 |
| MVUA | 294.74 | 3,684.25 | 118.22 |
| KUCHELEWA KWA MAJANI KIWANDANI | 91.50 | 1,143.75 | 39.51 |
| MATENGENEZO (REHABILITATION) | 1,921.30 | 24,016.25 | 822.72 |
| **JUMLA** | **7,065.27** | **88,315.88** | **2,895.96** |




**4.0. MAFANIKIO YA UZALISHAJI**

Pamoja na kuwepo na changamoto zilizo tajwa hapo juu, pia Kampuni imeshuhudia mafanikio katika maeneo makubwa mawili:-

a. Upande wa wadau wetu (yaani AMCOS na wakulima)
b. Upande wa kampuni

A. **Upande wa wadau wetu (yaani Mkulima na AMCOS)-**Pamoja na kusimamisha mitambo ya usindikaji kwa vipindi mbali mbali kupisha kipindi cha ukarabati mkubwa kampuni imeweza kugusa uchumi wa mkulima na vyama vyao vya Ushirika unaenda juu kutokana uzalishaji uliofanywa katika kipindi cha Sisalana kama ifuatavyo:-

- Kuongeza uzalishaji wa singa za majani ya mkonge (kwa kiasi na ubora)-pamoja na kwamba malengo ya Kampuni hayakufikiwa kutokana na chanagamoto zilizoainishwa hapo juu pia Kampuni ilijitahidi kuhakikisha hairudi nyuma kutokana na sababu hizo .Hivyo imeweza kuzalisha kiasi cha tani 4609.82 kutoka katika jumla ya meta za majani ya mkonge 140,286.78 kwa mwaka 2021 ikiwa ni ongezeko la **tani 453.46** kutoka katika tofauti ya meta 15,324.25 kwa kipindi cha mwaka 2020. Ongezeko hilo pia limeenda sambamba na uwepo wa madaraja ya juu yalioongezeka kiuzalishaji na yaliopungua kiuzalishaji mfano katika kipindi cha 2020 uzalishaji wa 3L , 3S, UG ilikuwa ni asilimia 53.07 (3L=0.05% na UG=53.02%) kutoka uzalishaji wa tani 4156.36 ukifananisha na mwaka 2021 ambapo uzalishaji wa 3L,3S na UG ni jumla ya asilimia 79.28% (3L=4.65%,3S=1.35% na UG=73.28%) kutoka uzalishaji wa tani 4609.82

- Kuongeza mapato ya mkulima na Vyama vya ushirika -kupitia usindikaji wa meta zaidi na madaraja ya 3L, 3S na UG kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na uzalishaji wa mwaka 2020. Hali hii imepelekea pato ghafi la mkulima kuongezeka zaidi tofauti na kipindi cha 2020.

  Takwimu za mapato kwa vyama vya ushirika na Wakulima limeambatanishwa katika jedwali namba 5 na 6 hapo chini.

**Jedwali namba 5: Mapato ya AMCOS (Ongezeko la Sh 76,621,360.00)**

| AMCOS REVENUES | | | |
|---|---|---|---|
| AMCOS | 2020 | 2021 | DIFFERENCE |
| | 5,000.00 | 5,000.00 | |
| HALE | 118,787,500.00 | 136,120,000.00 | 17,332,500.00 |
| NGOMBEZI | 100,787,500.00 | 107,497,500.00 | 6,710,000.00 |
| MAGUNGA | 105,100,000.00 | 108,247,500.00 | 3,147,500.00 |
| MAGOMA | 151,030,000.00 | 202,295,000.00 | 51,265,000.00 |
| MWELYA & USAMBARA | 149,107,540.00 | 147,273,900.00 | (1,833,640.00) |
| TOTAL | 624,812,540.00 | 701,433,900.00 | 76,621,360.00 |

**Jedwali namba 6: Mapato ya Wakulima (Ongezeko la Sh. 5,516,857,900.00)**

| GROSS REVENUES | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **GRADES** | **3L** | **3S** | **UG** | **SS UG** | **TOW I** | **TOW II** | **UF** | **TOTAL** |
| | **PRICE PER GRADES** | | | | | | | | |
| **2020** | HALE | - | - | 873,414,500.00 | 609,335,000.00 | 21,105,000.00 | 22,800,000.00 | 961,603,000.00 | 2,488,257,500 |
| | NGOMBEZI | - | - | 185,297,000.00 | 214,055,000.00 | 15,666,000.00 | 5,200,000.00 | 478,914,000.00 | 899,132,000 |
| | MAGUNGA | - | - | 359,440,200.00 | 320,205,000.00 | 15,678,000.00 | 6,280,000.00 | 833,840,000.00 | 1,535,443,200 |
| | MAGOMA | - | - | 1,235,013,500.00 | 834,940,000.00 | 25,605,000.00 | 33,200,000.00 | 1,389,128,000.00 | 3,517,886,500 |
| | MWELYA & USAMBARA | - | - | 1,134,089,600.00 | 553,731,800.00 | 31,957,500.00 | 4,520,000.00 | 1,148,979,000.00 | 2,873,277,900 |
| | **TOTAL GROSS REVENUES** | - | - | 3,787,254,800 | 2,532,266,800 | 110,011,500 | 72,000,000 | 4,812,464,000 | 11,313,997,100.00 |
| | | | | | | | | | |
| | **GRADES** | **3L** | **3S** | **UG** | **SS UG** | **TOW I** | **TOW II** | **UF** | **TOTAL** |
| | **PRICE PER GRADES** | | | | | | | | |
| **2021** | HALE | 104,697,500 | 801,762,500 | 1,015,250,000 | 717,328,200 | 243,270,750 | 28,060,500 | 716,377,500 | 3,626,746,950 |
| | NGOMBEZI | 17,425,000 | 599,637,500 | 444,275,000 | 329,205,200 | 58,768,150 | 17,087,000 | 458,562,500 | 1,924,960,350 |
| | MAGUNGA | 591,737,500 | 490,875,000 | 376,825,000 | 395,617,800 | 39,863,550 | 9,424,000 | 440,725,000 | 2,345,067,850 |
| | MAGOMA | 9,078,750 | 1,788,325,000 | 1,313,325,000 | 1,206,408,000 | 207,373,500 | 33,027,500 | 1,136,900,000 | 5,694,437,750 |
| | MWELYA & USAMBARA | 137,371,250 | 737,660,000 | 797,420,000 | 794,283,650 | 120,844,200 | 1,846,000 | 650,217,000 | 3,239,642,100 |
| | **TOTAL GROSS REVENUES** | 860,310,000 | 4,418,260,000 | 3,947,095,000 | 3,442,842,850 | 670,120,150 | 89,445,000 | 3,402,782,000 | 16,830,855,000.00 |

## B. Upande wa Kampuni

- ❖ Kufanikiwa kuhakikisha huduma ya uzalishaji inaendelea kuwa ya uhakika na yenye ubora katika kipindi chote, hii imejidhihirisha kwenye ongezeko la uzalishaji kwa kiasi na ubora wa madaraja ya juu ya Mkonge kama ilivyoelezwa katika taarifa za uzalishaji hapo juu.

- ❖ Kuhakikisha mitambo ya usindikaji inakuwa katika uimara wa utendaji kwa nyakati zote na pale inapotokea hitilafu kushughulikiwa kwa haraka. Hii inajidhihirisha katika taarifa ya ukarabati wa mitambo iliyoambatishwa na taarifa hii.

- ❖ Kukamilisha upanuzi wa vichanja vya kuanikia singa ilikuongeza ufanisi katika shughuli za uzalishaji katika viwanda vyote.

- ❖ Kurejesha ari ya wafanyakazi viwandani kote kufanya kazi kwa moyo kwakuwa maslahi yao yanazingatiwa na kulipwa kama inavyostahili na kwa wakati.

- ❖ Kuweza kulipa stahiki zote muhimu kwa Serikali hususani kodi zote zinazohitajika kwa mujibu wa Sheria.

- ❖ Kufanikisha ziara ya Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga iliyofanyika Septemba 2021 katika Viwanda vyote vya Sisalana. Pamoja na mambo mengine alisisitiza umuhimu wa kukamilisha ukarabati wa mitambo kwa wakati, kutafuta teknologia ya kisasa katika usindikaji na pia kujitangaza biashara ya bidhaa za mkonge nje ya Tanzania.

## 5.0. MUELEKEO WA KAMPUNI

Kampuni imeshaanza kufanya upembuzi yakinifu ili kupata muelekeo wa uwekezaji katika viwanda vyake vyote. Upembuzi utahusisha tathmini ya teknologia ya usindikaji inayotumika sasa na kushauri muelekeo wake pia kutathimini tija na kushauri maeneo mengine mapya yanayohitaji kupelekewa huduma ya usindikaji.


Aidha, katika kipindi cha mwaka 2022 kampuni imelenga katika kuhakikisha malengo inayojipangia katika usindikaji mkonge inayatimiza na ikiwezekana kuyapita. Hii itaambatana na kuendelea kuimarisha mitambo na wataalamu wake ilikuweza kutoa huduma bora zaidi kupita ya mwaka 2021.

## 6.0. HITIMISHO

Usindikaji wa majani ya mkonge katika viwanda vyote saba (7) umelenga zaidi kukwamua kipato cha wakulima kwa kuhakikisha huduma wanayo pata inakuwa ya ubora na viwango vinavyoelekezwa kitaalamu kupitia wataalamu wetu wa ndani na wa nje.

Tungependa kutoa shukrani zetu kwa wadau wetu hususani wakulima wa mkonge, AMCOS, Bodi ya Mkonge Tanzania, Wizara ya Kilimo, Serikali ya Mkoa wa Tanga na Wilaya ya Korogwe bila kusahau wanahisa wetu Bodi ya Wadhamini ya NSSF na watendaji wote wa Sisalana katika sehemu zote kwa kushirikiana katika kufanikisha uzalishaji wenye tija na manufaa kwa uchumi wa wakulima na Taifa.

**Mkonge kwa maendeleo ya Mkoa Tanga na Taifa kwa ujumla.**



**Afisa Mtendaji Mkuu**